SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.20 NO. 2 2021
DOI: 10.51984/JOHS.V20I2.1398

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/index.php/johs



# Muziki Kama Kichocheo Cha Mwamko Wa Siasa Nchini Tanzania

Salem Mahmoud Abdulhadi Massoud

Department of Languages and African Studies, Faculty of Arts, Sebha University

**Keywords:**
Muziki
Siasa
Mwamko
wa kisiasa
katika

**A B S T R A C T**

IKISIRI: Muziki ni miongoni mwa kazi za sanaa zinazolenga kuburudisha, kuelimisha, kuonya, kuhamasisha, kuadili pamoja na kazi nyingine nyingi. Suala la siasa ni miongoni mwa mambo ya msingi yanayotakiwa kujadiliwa kwa mapana na kwa kina ili kuwahamasisha watu hususani vijana kuongeza ushiriki wao katika shughuli za kisiasa. Ni dhahiri kuwa muziki unaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kuibua mijadala ya kisiasa. Makala haya yanalenga kujadili kwa kina mchango wa muziki katika kuleta mwamko wa kisiasa miongoni mwa wananchi nchini Tanzania. Aidha, makala haya yataangalia dhima na mchango wa muziki katika kuleta mwamko wa kisiasa nchini Tanzania.

# الموسيقى كمحفز للصحوة السياسية في تنزانيا

سالم محمود عبدالهادي مسعود

قسم اللغات الأفريقية، كلية الآداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
الموسيقى
السياسة
الصحوة
السياسية
في

**الملخص**

الأسطورة: الموسيقى هي أحد الأعمال الفنية التي تهدف إلى الترفيه والتثقيف والتحذير والإلهام والأخلاق بالإضافة إلى العديد من الأعمال الأخرى. تعتبر قضية السياسة من القضايا الأساسية التي يجب مناقشتها على نطاق واسع وعميق من أجل تحفيز الناس ، وخاصة الشباب ، على زيادة مشاركتهم في الأنشطة السياسية. من الواضح أن الموسيقى يمكن أن تساهم بشكل كبير في ظهور النقاشات السياسية. تهدف هذه المقالة إلى مناقشة مساهمة الموسيقى بالتفصيل في نشر الوعي السياسي بين شعب تنزانيا. بالإضافة إلى ذلك ، ستلقي هذه المقالة نظرة على دور ومساهمة الموسيقى في نشر الوعي السياسي في تنزانيا.

## UTANGULIZI

Mwamko wa siasa ni kiungo muhimu katika kuhakikisha watu wanashiriki kikamilifu na kwa usawa katika michakato mbalimbali ya kisiasa inayobeba maamuzi juu ya mustakabali wao. Kwa tafsiri nyepesi, mwamko wa siasa ni uelewa wa shughuli za kisiasa.Makala haya yanafafanua mwamko wa siasa kama hali ya kufahamu kwa kina haki za kiraia, shughuli za kisiasa na ngazi mbalimbali za uongozi. Hartley, kama alivyonukuliwa na Saroha (2016) anaamini kwamba mwamko wa kisiasa ni pamoja na kufahamu kwa kina mazingira ambamo watu na taasisi mbalimbali hufanya kazi pamoja na kufahamu mambo yanayoweza kuathiri mustakabali kwa namna moja au nyingine. Muziki kama tawi la sanaa huangazia mambo mbalimbali ya kijamii, uchumi na hata mambo ya kisiasa kama Adebayo (2017) anavyounga mkono hoja kwa kudai kwamba muziki humulika mambo ya msingi katika jamii kama vile utamaduni na utaratibu mzima wa maisha ya wanajamii. Kwa mantiki hii, muziki unaweza kutumika kuleta mwamko wa kisiasa miongoni mwa watu fulani na kuwafanya waweze kuchukua hatua stahiki katika kuunga mkono au kupinga sera za kisiasa pamoja na maamuzi yanayoweza kuchukuliwa na serikali juu ya maisha yao.

Muziki umekuwa ukihusishwa na harakati za kisiasa tangu zamani. Historia inaonesha kuwa athari za ukoloni na utumwa katika baadhi ya mataifa kama Marekani zilipelekea kuibuka kwa wanaharakati walioanza kudai haki zao za msingi za kiraia kupitia sanaa mbalimbali ikiwemo muziki (Street, 2003). Hii inaonesha kwamba muziki ni miongoni mwa njia nzuri za uhamasishaji wa maswala mbalimbali ya kijamii. Neuman (2008) katika makala yake Music and Politics anamnukuu Hill akidai kwamba ‘muziki una nguvu ya kipekee ya uchochezi tofauti na jarida linaloandikwa kwani muziki husikilizwa pasipo na uhitaji wa kusoma na kutokana na burudani inayotokana na muziki, basi muziki hurudiwa kusikilizwa tena na

*Corresponding author:
E-mail addresses: sal.massoud@sebhau.edu.ly
*Article History : Received 15 August 2021 - Received in revised form 09 November 2021 - Accepted 15 December 2021*

tena na kujikuta ukihamasisha watu pasipo kutumia jitihada kubwa tofauti na jarida ambalo linaweza kusomwa mara moja na kuachwa'. Nchini Tanzania, muziki unaoasawiri mambo ya kisiasa ni ule wa HipHop. Tanzu nyingine za muziki husawiri sana mapenzi na maudhui mengine tofauti na siasa. Wasanii wanaofahamika sana kwa kusawiri siasa katika nyimbo zao ni Ibrahim Musa (maarufu kama Roma Mkatoliki), Mrisho Mpoto, Kala Jeremiah, Stamina, Joseph Haule (maarufu kama Professor Jay), Joseph Mbilinyi (maarufu kama Sugu au Mr. Two) na wengine wengi.Kupitia muziki wa HipHop, wasanii hawa wamekuwa wakileta mchango mkubwa katika kuleta mwamko wa kisiasa miongoni mwa watu wengi nchini Tanzania hususani vijana na kuwafanya waongeze ushiriki katika siasa.

**Dhima ya Muziki katika kuleta Mwamko wa Kisiasa.**

Makala haya yanaangalia kwa kina namna fani na maudhui ya muziki nchini Tanzania yanachochea mwamko wakisiasa miongoni mwa watu. Ni dhahiri kwamba wasanii hutumia vipengele vya fani na maudhui kwa namna mbalimbali ili kuibua yale yanayoendelea katika jamii yoyote ile. Kwong, (2016) anadai kwamba muziki una nguvu ya hisia ambayo huathiri akili na mwenendo wa watu kwa ujumla. Makala haya yanaunga mkono hoja hii kwa kuangalia namna muziki unaweza kuchochea mwamko wa kisiasa miongoni mwa watu kupitia muundo na maudhui ya mashairi ya nyimbo mbalimbali. Kupitia maudhui ya wimbo, msanii anaweza kuibua mwamko wa kisiasa kwa kuimba juu ya mambo mazuri au mabaya yanayofanywa na viongozi wa serikali husika. Kwa upande mwingine, fani huchochea mwamko wa kisiasa kutokana na uwezo wa kuwajaza wasikilizaji hisia mbalimbali juu ya maudhui ya wimbo. Kwa kuwa makala haya yamejikita katika muziki na mwamko wa kisiasa katika jamii za kitanzania, yatachambua mashairi ya nyimbo mbalimbali zinazosawiri siasa na namna mashairi hayo yanavyoleta mwamko wa kisiasa miongoni mwa watu. Katika kuchambua mashairi ya nyimbo hizo, makala haya yanaangalia maudhui yanayoguswa kama ifuatavyo.

**Matumizi mabaya ya fedha za umma**

Kila serikali hutenga bajeti na kuelekeza mafungu ya pesa katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Serikali bora huwa na viongozi wenye nidhamu na wanaotenda haki katika kutekeleza miradi ya maendeleo lakini serikali mbovu huwa na viongozi wenye tamaa na ubinafsi wanaoweka kipaumbele katika kutumia fedha za umma kwaajili ya kujinufaisha wao wenyewe. Wasanii wanaosawiri siasa katika nyimbo zao wamekuwa mstari wa mbele katika kuibua uelewa na ufahamu juu ya matumizi mabaya ya fedha za serikali. Kala Jeremiah na Roma katika wimbo wao 'nchi ya ahadi' wamesawiri barabara matumizi mabaya ya fedha za serikali kwa kuzungumzia mradi hewa wa Escrow ambao uliwanufaisha wanasiasa wachache kwa kutumia zaidi ya shilingi za kitanzania bilioni 300.

Ehee, umenikumbusha na Escrow, bilioni 300 hivi ziligawanwa vipi broi

Nilijua tu utauliza maana nahisi umetumwa,
kuhusu Escrow mmmh, haikuwa ni mali ya umma ila tupo kwenye mchakato,
Kwa hili tunajituma, kwanza hayo yalishapita,
Mbona unachochea ya nyuma?

Katika wimbo huu wa majibizano, tunaona Kala Jeremiah (anaesimama kama mwakilishi wa wananchi) anamuuliza Roma (anaesimama kama mwanasiasa) kuhusu matumizi ya fedha nyingi zilizopotea katika mradi hewa wa Escrow. Katika kujibu swali hili, Roma, anatoa majibu ambayo wananchi hawayaelewi na hawaridhiki nayo na ndiyo maana kwenye kibwagizo (chorus) wananchi wanapoulizwa 'Wapiga kura mnamsikia muheshimiwa?' wanajibu:

Eeeh tunamsikia lakini hatumuelewi,
Mwambie tumepigikaii tumechoka hatujielewi

Kwa kuzingatia mashairi hayo, tunaona kwamba Roma na Kala Jeremiah wamefanikiwa kuleta mwamko wa kisiasa miongoni mwa watu kwa kuibua dhamira ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Aidha, mbinu ya majibizano iliyotumika katika mashairi hayo imesaidia kuonyesha uhalisia wa wahusika kwani tunaona namna mwakilishi wa wananchi pamoja na wananchi wenyewe wanavyoongea kwa unyonge kutokana na hali ngumu ya maisha waliyonayo wakati mwanasiasa anajibu kwa jeuri na kwa kujiamini kwani yeye hajui kabisa hali ya umaskini na madhara yake. Mtindo wa majibizano katika mashairi haya unahamasisha na kuamsha watu juu ya uovu unaofanywa na baadhi ya watumishi wa serikali na hivyo wananchi wanapata mwamko wa kisiasa na kuanza kujijengea tabia ya kuhoji juu ya matumizi ya fedha za umma.

Vilevile, namna kibwagizo cha wimbo kilivyoundwa inatia hamasa kubwa na kuwafanya watu wapate mwamko wa kisiasa kutokana na hisia kali inayooneshwa na wananchi katika kumjibu muheshimiwa ambaye katika mashairi hayo anasimama kuwakilisha kundi la wanasiasa wachache waliojawa na tabia ya ubadhilifu wa fedha za umma.

**Ahadi za Kampeni**

Ni kawaida kwa kila mwanasiasa kutoa ahadi wakati wa kampeni kwa lengo la kushinda nafasi ya uongozi kwani wananchi humchagua wakiwa na matumaini makubwa kwamba ahadi alizoweka atazitimiza pindi anapokuwa madarakani. Vyama vya siasa pia huweka ahadi kupitia ilani na utekelezaji wa ahadi hizo hufanyika pindi chama kinapokuwa madarakani. Baada ya uchaguzi, chama cha siasa au wanasiasa wanaoibuka washindi katika nafasi mbalimbali za uongozi husahau utekelezaji wa ahadi zao na hivyo kujikuta wanawakosesha wananchi haki zao za msingi. Katika hali kama hii, muziki nchini Tanzania huwa na nafasi kubwa sana katika kuwakumbusha viongozi juu ya ahadi walizozisahau au kuzipuuzia. Katika wimbo uleule 'nchi ya ahadi' ulioimbwa na Roma na Kala Jeremiah tunaona mwakilishi wa wananchi akimuuliza muheshimiwa juu ya ahadi alizoahidi wakati wa kampeni.

Uliwaahidi wamama wodi ya wazazi,
Walimu hawajasahau ile ahadi ya makazi,
Vipi kuhusu viwanda ndani ya makazi
Pia vitu kupanda bei, muheshimiwa tuweke wazi

Vitu kupanda bei ni mfumo wa dunia nzima
Na kuhusu wodi ya wazazi nitalifatilia kwa kina
Hata mimi ni binadamu jamani naumia pia
Nikitazama wanavyoishi walimu nasikia kuliaaa

Majibu yako tu yanaonesha umetingwaiii
Unakumbuka kijiji ulichoahidi daktari bingwa ?

Kusema kweli sina kumbukumbu fresh
Ila safari hii anakuja namlipa pesa yake cash
Mi nadhani huu sio muda wa kulaumiana
Hebu punguza maswali, kwanza vipi umeshakula kijana?

Kwa kurejelea mashairi ya wimbo huu, ni dhahiri kuwa waimbaji wanajaribu kuwakumbusha wananchi kuwa na utamaduni wa kuwahoji wanasiasa juu ya ahadi ambazo hazijatekelezwa kwa sababu mbalimbali. Mashairi ya namna hii yanaibua hisia kali kwa wananchi na kuwafanya waanze kufatilia mwenendo wa viongozi wao na hivyo kujikuta na mwamko wa hali ya juu kuhusiana na siasa ya nchi.

**Kujimilikisha na kujilimbikizia mali za Umma**

Muziki nchini Tanzania unaangazia sana suala la watumishi wa umma kujimilikisha mali za umma bila kibali chochote kutoka serikalini. Kujimilikisha mali za umma ni kitendo cha kutwaa mali yoyote inayomilikiwa na umma (ardhi, majengo, viwanda na miundombinu mingine) kutokana na nguvu ya cheo cha mtumishi fulani. Hii ni moja ya tabia zinazokwamisha maendeleo ya umma na kufanya wananchi kuwa na hali duni ya kiuchumi kila mara. Wasanii wa muziki nchini Tanzania hawajafumba mdomo dhidi ya tabia hii kwani wamekuwa wakiimba nyimbo zinazolenga kuibua maovu ya namna hii na kuwafanya wananchi wengine kuwa na mwamko wa kisiasa. Mrisho Mpoto katika wimbo wake 'Nikipata Nauli' anasawiri namna wanasiasa wanavyowadhulumu wananchi wa tabaka la chini kwa kujimilikisha na kujilimbikizia mali za umma kwaajili yao na koo zao pekee.

Mjomba, tazama maisha yetu,
Utadhani mchezo wa kuigiza,

Migodi sita, yote ya kwangu,
Hekari mia moja, najiandaa kustaafu nipate sehemu ya kupumzika
Maziara je?
Aaah, alimuoa mtoto wa mjomba wangu, kaka yake na mama yangu,
Nikampa zawadi,
Inauma sana, inauma sana kugawa malalio iv yetu kama zawadi mjomba"

Mashairi haya yanatia hamasa ya kutaka kupigania haki. Katika mashairi hapo juu, Mpoto anafichua wazi namna viongozi wa serikali wanavyojilimbikizia mali kama vile migodi na ardhi kwaajili yao binafsi pamoja na ndugu zao. Namna Mrisho Mpoto anavyowasilisha dhamira ya kujilimbikizia mali kwa baadhi ya wanasiasa inatia uchungu na kufanya watu wenye maisha ya chini kuamka na kuanza kupigania usawa kwa njia za amani au zisizo za amani ilimradi haki ipatikane. Hivyo basi ni dhahiri kuwa muziki una nguvu kubwa sana ya ushawishi na unaweza kuleta mwamko wa kisiasa miongoni mwa watu ikiwa wasanii watasawiri barabara mambo mema na mabaya yanayotendwa na wanasiasa.

**Unyanyasaji na matumizi ya mabavu**

Wasanii wa muziki nchini Tanzania wamegusia juu ya unyanyasaji wa raia unaofanywa na polisi na vyombo vya dola kwa ujumla. Ni wazi kwamba serikali imekuwa ikitumia jeshi la polisi kuvuruga maandamano na mikutano ya watu mbalimbali wanaodai haki zao au wakati mwingine hutumia jeshi la polisi kukamata baadhi ya wanaharakati na kuwasulubisha kwa lengo la kuwakandamiza na kuwanyamazisha. Kitendo hiki kimekuwa kikilaaniwa na watu wanaofahamu tabia hiyo inayofanywa na serikali tawala lakini wasanii wanaleta mwamko kwa watu wengi zaidi kwa kuimba dhamira kama hizi. Mrisho Mpoto katika wimbo wake 'Nikipata Nauli', anatumia mistari michache kuuelimisha umma juu ya matendo ya kikatili yanayofanywa na polisi:

Nikipata nauli, ntakuja kukunong'oneza mjomba
Please, tafadhali, acha maagizo mlangoni
Maana siku hizi wanataka sifa kweli, hawachagui pa kupiga
Utasikia "ririkuwa rikipambana na porisi tukarishindav*"
Waapi! Kumbe mpwao na mipango ya kuinusuru nchi
Mpaka zikikufikia wewe, huku tiamaji tiamaji
Tahamaki uchaguzi huo….
Natania tu mjomba, ila kweli
Nikipata nauli nitakuja

Mashairi haya yanaonesha namna msanii alivyotumia fani kuibua ukatili wa polisi dhidi ya raia. Msanii ametumia mbinu ya kejeli kwa kuhusianisha lafudhi mbaya na maaskari polisi.Hii inaonesha jinsi gani msanii anachukizwa na matendo ya askari polisi ya kupiga raia pasipo sababu za msingi. Kupitia mashairi haya, msanii anachochea mwamko miongoni mwa watu ili watambue kinachofanywa na maaskari polisi.

Katika wimbo wa 'Zimbabwe' Roma anafichua pia matumizi ya vyombo vya dola katika kunyanyasa wananchi. Katika tukio la kweli lililomtokea, Roma anadokeza namna alivyoteswa baada ya kutekwa na kupekelekwa mahali kusiko julikana.

Wengi mlijiuliza waloniteka ni maaskari
Mkanitafuta vituo vyote Central hadi Sitaki shari,
Wakasema hawajui nilipo, mama alienda hadi mortuary dah!

Mashairi haya yanadhihirisha kuwa vyombo vya dola vinatumika kuwateka na kuwanyanyasa wanaharakati. Kwa kuibua maovu haya, anawahamasisha wananchi kuwa makini sana na uonevu unaofanywa na baadhi ya maofisa wa serikali. Roma anaongeza katika mashairi kwa kueleza mambo aliyofanyiwa akiwa mateka.

Nilipokuwepo sikuwa najua hii saa nne hii saa nane,
Nilichohitaji nitoke mzima na ndugu zangu tuonane,
Nimechapwa mijeledi, nimevunjwa bila huruma,
Asante mliopaza sauti nimeiona nguvu ya umma,
Siku tatu nimefungwa macho, mikono imefungwa nyuma'

Katika mashairi, Roma anaeleza kuteswa bila huruma lakini anawapongeza wananchi waliopaza sauti juu ya kutekwa kwake. Hii inapelekea kuchochea mwamko wa kisiasa miongoni mwa watu.

**Kusifu Maendeleo**

Mwamko wa kisiasa unaweza ukaletwa hata kwa kusifu juhudi wanazofanya baadhi ya viongozi katika kuleta maendeleo ya nchi. Wasanii nchini Tanzania husifia pale viongozi wanapofanya juhudi za kuleta maendeleo kwa nchi nzima. Msanii kama Harmonize alishindwa kuzuia hisia zake katika kutambua mchango wa Rais Magufuli katika maendeleo nchini Tanzania. Harmonize katika kutaja miradi ya maendeleo iliyosimamiwa na Rais Magufuli anamsifu kwa kusema,

I wish ningemuona magufuli, nipige magoti
Nimpongeze hadharani,
Yaani Rais wa Jamuhuri ya muungano,
Mchapa kazi, hachoki, anaepinga nani?
Ametuvusha vikwazo, wewe na mimi,
Ona nchi anavyoijenga
Flyover sasa tunazo, daraja la Kigamboni,
Airport imeshajengwa
Acha nikupongeze kwa Air Tanzania,
Zidi baba utuongeze Airbus, Bombadier l
Standard gauge tuteleze, kusafiri unasinzia,
Acheni tu niwaeleze, Magufuli kapania….

Mashairi kama haya yanawafumbua macho watu ambao hawana imani na kiongozi fulani lakini pia kuwaonesha juhudi zinazofanywa na viongozi katika kuleta maendeleo. Kwa kurejelea mashairi hayo juu, ni dhahiri kuwa wasanii wanachangia kwa kiasi kikubwa katika kutoa mwamko wa kisiasa miongoni mwa watu. Kusifu juhudi za serikali katika kuleta maendeleo au kumsifu kiongozi anaefanya vizuri huchagiza mwamko wa kisiasa na kufanya viongozi wengine waone kwamba wana wajibu wa kufanya vizuri pia katika shughuli za kiserikali za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

**Hitimisho**

Makala haya yanahitimisha kwa kudai kwamba muziki una nafasi kubwa sana katika kuleta mwamko wa kisiasa kwani kupitia fani na maudhui, wasanii husuka nyimbo zao kitaalamu na kugusa hisia za wasikilizaji kitu ambacho huwafumbua macho na kuwapatia mwamko juu ya mambo yanayofanyika nchini.

Diskografia na Marejeleo


Roma, (2018). Zimbabwe. Dar es Salaam: Tongwe Records Production

Harmonize, (2019). Magufuli. Dar es Salaam: Wasafi Records Production

Mrisho Mpoto ft Banana Zoro, (2016). Nikipata Nauli. Dar es Salaam: Soround Sound Studio

Kala Jeremiah ft Roma (2015). Nchi ya ahadi. Dar es Salaam: Plexity Records

Neuman, D. (2008). Music & Politics in the Classroom: Music, Politics and Protest 1-2. https://dx.doi.org/10.3998/mp.9460447.0002.205

Saroha, J.K. (2016). The political Awareness among Youth: 2250-0758.574-576. Retrieved from https://www.ijemr.net/DOC/ThePoliticalAwarenessAmongYouth.pdf

Street, J. (2003). 'Fight the Power': The Politics of Music and the Music of Politics. Blackwell Publishers. UK. Retrieved from https://www.cambridge.org/core/journals/government-and-opposition/article/fight-the-power-the-politics-of-music-and-the-music-of-politics/73F8C284A51814A3F6193402BF9F806C

Onyebadi, U. (2018). Political Messages in African Music: Assessing Fela Anikulapo-Kuti, Lucky Dube and Alpha Blondy. Retrieved from https://www.mdpi.com/2076-0787/7/4/129/pdf

Kwong, M. (2016). "The Impact of Music on Emotion: Comparing Rap and Meditative Yoga Music." *Inquiries Journal/Student Pulse*, *8*(05). Retrieved from http://www.inquiriesjournal.com/a?id=1402 accompany your final submission.